

## Historia ya ushirikiano

- 1981 Mchungaji Mwakasyuka toka Tukuyu alitambua bidii ya waumini wa jumua za Ulm, ili kuunda ushirikiano kati yao na kanisa la Moravian Tukuyu – Tanzania.
- 1986 Mwanzoni ushirikiano ulikuwa hasa kati ya kikundi cha vijana wa Wiblingen na wajumbe wa uwakilishaji wa jumua hizo. Mwaka huo huo vijana sita toka jimbo la Ulm walitembelea Tukuyu kufuatia mwaliko wa kikundi cha vijana wa Tukuyu.
- 1988 Wawakilishaji sita wa kikundi cha vijana wa Tukuyu walitembelea jumua za Ulm kwa muda wa wiki nne.
- 1989 Baada ya kurejea mchungaji Hauff toka Chuo cha Theologia Mbeya, jumua ya Dornstadt ilijiunga na ushirikiano
- 1991 Kwa mara ya pili wajumbe wa jumua za Ulm walitembelea Tukuyu. Mwaka huo pia mradi wa ng'ombe wa waziwa ulianzishwa.
- 1993 Kutembelea kwa wajumbe toka jumua ya Tukuyu kwa mara ya pili kuliimarisha mawasiliano katika ngazi ya kikazi na kibinafsi. Mwaliko wa kutembelea Tukuyu katika mwaka wa 1995 uliwakilishwa.
- 1995 Kwa ziara ya tatu wageni kutoka Ulm walikuwa kualikwa pia na shirika za Makandana, Ndembela na Lumbila ambazo zinajitegemea na ushirika wa Tukuyu sasa.
- 1997 Kwa mara ya tatu washirika sita toka Tukuyu walikuwa wageni wetu, na kilele cha safari hii ilikuwa sikukuu ya makanisa (Deutscher Evangelischer Kirchentag) huko Leipzig, kukutana na wafuasi wa „Brüdergemeine“ huko Herrnhut.
- 1999 Kwa mara ya nne kikundi cha watu toka katika jumua zetu walitembelea Tukuyu na ni mara ya kwanza katika matembeleano yote, walipata malazi katika familia za watu binafsi.
- 2001 Kwa mara ya nne wageni toka Tukuyu wametembelea. Mambo muhimu katika msafara huu ilikuwa sikukuu ya makanisa (Kirchentag) huko Frankfurt, majadiliano maalum katika nyumba ya starehe „Schlössle Erbsetten“ kusherehekea miaka ishirini ya ushirikiano.
- 2003 Tulipata nafasi ya kuongea vizuri na wazi na makundi yote ya ushirika. Mazungumzo haya yalikuwa muhimu sana wakati wa safari hii ya tano ya wajumbe kutoka Ulm kwenda Tukuyu.
- 2005 Wakati wa safari ya tano ya wajumbe kutoka Tukuyu wageni hao walipata nafasi ya kuonana na watoto na vijana katika session zao na pia katika Shule na katika masomo ya kipa imara. Tuliongea kuhusu njia ya kuwapa vijana nafasi ya kuijunga na makundi ya wasafiri.
- 2007 Mikutano na vijana na mazungumzo juu ya vichwa mbali mbali kama "ujana na kanisa", "afya", "haki duniani" vilikuwa mikazo ya ziara ya wajumbe wa Ulm katika Tukuyu. Mwanzoni kundi la Ulm lilika katika "nyumba ya wageni", baadaye wageni walikaribishwa kibinafsi



*Wajumbe kutoke Ulm 2003 wanakaribishwa na Mwenyekiti wa Kanda la Kati, Mch. Mwakipesile.*

*Delegation aus Ulm 2003 in Tukuyu beim Empfang bei Herrn Dekan Mwakipesile.*

## Uzoefu na matumaini njiani mwa ushirikiano.

Muhimu kwetu ni kwamba watu wenye mila na desturi tofauti ambao ni wafuasi wa dini moja wawe na nafasi ya kuweza kuonana. Katika mwananano huo tunapata ujuzi juu ya tofauti hizo katika maisha ya kiuchumi na kimila. Tunawasiliana katika lugha ya Kiingereza, Kiswahili, bila maneno na katika musiki. Tunaelimishana kati yetu, tunasali pamoja, tupo pamoja njiani kwenye nyumba zetu na katika vikundi vyetu. Kwa wakati huu tunasaidia katika ujenzi wa hosteli ya kikundi cha wanawake Tukuyu, pia katika mradi wa kushona nguo, tukiwafunza wanawake na wanaume ushonaji na ukataji wa nguo.

Anwani ya kamati ya ushirikiano:

Tukuyu Moravian Church  
P.O. Box 26  
Tukuyu, Tanzania  
Tel.: 00255-25-2552148

## Partnerschaft Tukuyu-Tansania Ulm-Deutschland

Folgende Gemeinden sind an der Partnerschaft beteiligt:

**Tukuyu** - **Dornstadt  
Grimmelfingen  
Erbach  
Söflingen  
Wiblingen**

Herrnhuter Brüder-  
gemeine - Tukuyu  
Moravian Church  
in Tanzania

Gemeinden des Dekanats  
Ulm – Evangelische  
Landeskirche  
in Württemberg

**Tukuyu (Tansania) mit Lage auf dem  
afrikanischen Kontinent**

© *Tukuyu*

